**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**S. L.P 30261**
**Simu:**
**Nukushi:**
**(023) 2402657**
**Barua pepe: rbcpwani@pccb.go.tz**
**Wavuti : www.pccb.go.tz**

# TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

**PWANI-JULAI 15, 2020**

## TAKUKURU MKOA WA PWANI YAFANYA KAZI KWA KASI KWA LENGO LA KUSAIDIA WANYONGE NA KUINUA HALI ZAO KIUCHUMI

**Ndugu waandishi wa habari,**

Nimewaalikeni kuja hapa ili kupitia kwenu, Watanzania wote wafahamu kazi zilizofanywa na TAKUKURU Mkoa wa Pwani kwa kipindi cha Mwezi Aprili mpaka Juni, 2020. Na ikumbukwe kuwa ni utaratibu wetu kufanya hivyo ili umma wa watanzania wafahamu tunafanya nini na watuelewe kwa kuunga mkono juhudi za mapambano dhidi ya Rushwa nchini.

Kwa msingi huo naomba kuainisha kazi zilizofanywa na TAKUKURU Mkoa wa Pwani kwa kipindi hicho kama ifuatavyo:

### UCHUNGUZI NA MASHITAKA

- Kupitia Ofisi ya TAKUKURU kituo maalum cha Chalinze tuliweza kuokoa na kumrejeshea fedha Taslimu kiasi cha Shilingi 4,900,000/= Mwalimu Mstaafu aitwae YUSUPH RASHID KIMWERI ambaye alikuwa amelipa kwa Bw. IBRAHIM MAREMA MASWE kupitia mkopo usiofuata sheria, kanuni na taratibu zinazosimamiwa na taasisi za fedha nchini maarufu kama "***mkopo umiza***" wa kiasi cha Shilingi 700,000/= aliokopa mwaka 2018 na kupitia riba deni kukua na kufikia Shilingi 13,000,000/= ambalo Mstaafu huyo alilipa mara baada ya kupokea pensheni yake ya kustaafu tarehe 27 mei 2020.

- TAKUKURU baada ya kupata malalamiko juu ya mkopo huo tulifanya uchunguzi wa kina na kubaini kwamba mtuhumiwa alifanya biashara ya kukopesha fedha kinyume na

kanuni ya 4 ya "Microfinance Act" ya Mwaka 2019. Aidha baada ya mtuhumiwa kutambua kosa aliahidi kurejesha fedha hizo Mtuhumiwa ameanza kurejesha fedha hizo mpaka sasa amesharejesha kiasi cha Tshs. 4,900,000/-na mtuhumiwa bado anatakiwa kurejesha kiasi cha Shilingi 8,100,000/= kilichobaki.

- Aidha, TAKUKURU imeweza kuokoa fedha kiasi cha **Shilingi 35,000,000/=** kati ya Shilingi 394,156,335.30 ambazo ni fedha za malipo ya korosho kwa wakulima mkoani Pwani. Kwani kampuni ijulikanayo kama MAFUBILO GENERAL SUPPLIES LTD ya jijini Dar Es Salaam ilinunua kwa mkopo korosho wa wakulima kupitia AMCOS za Visiga, Misugusugu, Kongowe, Mwendapole, Mkombozi na Miembe saba zenye jumla ya Shilingi 394,156,335.30 hivyo Malipo ya korosho hizo yalisuasua mpaka TAKUKURU ilipofanyia kazi na kuhakikisha mnunuzi analipa. Na mdaiwa amepewa maagizo ya kulipa mpaka amalize deni lote haraka iwezekanavyo ili wakulima wapate haki yao.

- Aidha TAKUKURU wilaya ya Kibiti iliweza kuokoa na kurejesha kwa wakulima fedha kiasi cha **Shilingi 52,000,000/=** zilizotokana na mauzo ya korosho za wakulima wilayani humo **tani 65,000** kwa kampuni ya **CDJKL NUTS** ambayo iliingia mkataba wa kununua korosho hizo tarehe **16 Machi 2020** kwa makubaliano ya kuwalipa wakulima hao baada ya mwezi mmoja, hata hivyo kampuni hiyo haikutekeleza makubaliano hayo kwa kisingizio kwamba wanunuzi wa korosho hizo toka India wapo ***"Lock down"*** kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa korona yaani **COVID 19.**

- TAKUKURU wilayani Chalinze pia ilifanikiwa kumrejeshea shamba lenye ukubwa wa heka moja Mkazi wa Msoga Bi. ZAWADI TENGENEZA ambalo ilidaiwa kudhulumiwa na Baraza la Ardhi la kata ya Msoga kwa kutoa hukumu ya shauri lake kwa kumpa haki Bw. RAJABU YUSUFU NZOGORO kinyume na taratibu. Baada ya TAKUKURU kuingilia kati Baraza hilo lilimrejeshea shamba lake ambapo awali ilidaiwa Baraza lilipindisha taratibu kufuatia mmoja wa wanasiasa kuingilia kati shauri kwa kununua shamba hilo.

- Pamoja na kurejesha ardhi hiyo TAKUKURU kupitia Ofisi ya wilaya ya Kisarawe imefanikiwa kurejesha kwa wananchi wa Kijiji cha CHAMALALE ardhi yenye ukubwa Ekari 20. Ardhi hiyo iliyopo katika kitongoji cha Kilimani, Kijiji cha CHAMALALE

iliuzwa kwa mtu aliyejiita mwekezaji kwa gharama ya Tsh 10,000,000/= na Viongozi wa kijiji hicho kwa kushirikiana na mtu mmoja aitwae Bw. SAID MUHUNZI ambaye si mkazi wa kijiji hicho. Watuhumiwa walipokea kiasi cha Tsh 7,000,000/= kama malipo ya awali ya mauzo ya ardhi hiyo kinyume na taratibu. Baada ya TAKUKURU kuanza uchunguzi ilibaini eneo hilo ni mali ya kijiji hivyo eneo hilo lililazimika kurudi mikononi mwa kijiji kupitia mkutano mkuu wa wananchi.

- TAKUKURU wilaya ya Rufiji iliendelea kufanya uchunguzi juu ya ubadhirifu wa fedha kupitia Chama cha Ushirika cha msingi cha NGARAMBE AMCOS, Uchunguzi umebaini kwamba kati ya **Shilingi 31,750,800**/= ambazo chama kilipaswa kupata kama faida, kiasi cha **Shilingi 17,462,000/=**kililipwa na Afisa Mtendaji wa Kata ya ngarambe aitwae SARAH FULGENCE kupitia wakulima hewa ambapo aliingiza majina ya TANZANIA COMMOCITIES TRADING COMPANIES LTD na MAGDALENA EUGINE KULLAYA na kupelekea hasara ya kiasi cha **Shilingi 17,462,000/=** na kiasi cha **Shilingi 625,000**/= kililipwa kwa SUDI KIDAGAA ambaye hakuuza ufuta kwa chama hicho, jina ambalo liliingizwa na JAFARI KIDAGAA katika orodha ya malipo. Na hivyo kupelekea chama cha msingi kupata hasara ya Shilingi **18,087,600/=.** Pamoja na uchunguzi huo tayari wahusika wamepewa amri ya kurejesha fedha hizo kwa chama haraka iwezekanavyo na tayari Bi. SARA FULGENCE ameshaerejesha **Shilingi 3,000,000/=** ambazo zimewekwa kwenye akaunti ya Halmashauri ya wilaya ya Rufiji na mpaka kufikia mwezi Agosti, 2020 fedha hizo zitakuwa zimerejeshwa katika chama.

- **Shilingi 4,032,000/=,** ni fedha zilizorejeshwa na baadhi ya wakulima na viongozi wa chama cha ushirika cha KILIMANI kilichopo wilaya ya Rufiji ambao walifanya ubadhilifu wa fedha zilizokuwa zinapaswa kulipwa kwa wakulima halali waliouza kororsho zao kwa msimu wa mwaka 2018/2019.

- TAKUKURU wilayani Rufiji pia iliokoa kiasi cha **Shilingi 8,000,000/=,** kutokana na operesheni iliyofanywa kwa ushirikiano na wakala wa Huduma za Misitu nchini yaani TFS fedha hizo zinatokana na faini kwa baadhi ya wafanyabiashara wa magogo kukiuka taratibu za uvunaji ikiwemo kuvuna katika hifadhi, kutokuwa na vibali vya uvunaji na kuvuna magogo yasioruhusiwa.

- Katika kipindi cha robo ya mwisho ya mwaka TAKUKURU wilaya ya Mafia imefanikiwa kuokoa jumla ya fedha Shilingi **16,450,745/=** ambazo zilikusudiwa kuchepushwa na baadhi ya watumishi na mawakala katika Halmashauri ya wilaya ya Mafia wenye dhamana ya kukusanya ushuru kwa kutumia mashine za kieletroniki "Point Of Sale".

- Aidha, jumla ya **kesi 31** ziliendelea kuendeshwa katika mahakama mbalimbali za mkoa wa Pwani ambapo **kesi 2** zilitolewa hukumu ambapo upande wa Jamhuri ulishinda kesi zote mbili kwa washitakiwa kuamuliwa kufungwa jela au kulipa faini ambapo katika kesi ya kwanza mshitakiwa ambaye alikuwa Afisa Tawala wa wilaya ya Kisarawe alihukumiwa kifungo cha miaka mitano kwa kila kosa au kulipa faini ya Shilingi 1,000,000/= kwa kila kosa ambapo alishitakiwa kwa makosa mawili. Hivyo mshitakiwa alilipa faini ya shilingi 2,000,000/= na pia aliamuliwa kurejesha kwa mlalamikaji kiasi cha fedha za Rushwa kilichobaki baada ya kuanza kumrejeshea fedha mlalamikaji.

- Na katika kesi ya pili mshitakiwa ambaye alikuwa ni Mwenyekiti wa kijiji aliyeshitakiwa kwa kosa la kuomba na kupokea Rushwa ya Shilingi 100,000/= toka kwa mlalamikaji ili mshitakiwa asiende kutoa ushahidi katika kesi ya jinai iliyokuwa inamkabili ndugu wa mlalamikaji. Katika kesi hiyo mshitakiwa alihukumiwa jela miaka mitatu kwa kila kosa au kulipa faini ya Shilingi 500,000/= kwa kila kosa na hivyo mshitakiwa alilipa faini ya Shilingi 1,000,000/= kwa makosa yote mawili.

Hayo ni matunda ya jamii kuielewa TAKUKURU na kutoa ushirikiano katika mapambano dhidi ya Rushwa hususani katika utoaji wa taarifa na ushahidi mahakamani.

Ofisi ilipokea malalamiko **197** kati ya hayo malalamiko **133** uchunguzi wake unaendelea katika hatua mbalimbali na malalamiko **64** yalionekana kuangukia katika sheria nyinginezo hivyo walalamikaji walishauriwa na kuelekezwa sehemu husika kwa lengo la kutatua kero zao.

**ELIMU KWA UMMA.**

**Ndugu waandishi wa habari,**

Pamoja na uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa korona, ofisi iliendelea kutoa elimu kwa jamii kwa njia mbalimbali za uelimishaji ikiwemo njia ya mtandao kupitia Whatsapp. Katika kipindi hicho jumla ya semina **9** zilitolewa, mikutano **7** ilifanyika, maonesho **2** yalifanyika na vipindi **5** vya redio vilifanyika.

Elimu tuliyotoa ilihusiana na Madhara ya Rushwa katika chaguzi za kisiasa, Rushwa ya Ngono na Umuhimu wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo, hivyo tuliweza kuwafikia jumla ya wananchi 1210.

**UZUIAJI RUSHWA**

Katika eneo la Uzuiaji Rushwa tulifanya uchambuzi wa mifumo 06 katika maeneo mawili ambayo ni; mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa vyama vya msingi vya ushirika (AMCOS) na TARURA). Malengo ya kufanya uchambuzi wa mifumoni kubaini mianya ya rushwa na kutafuta mbinu za kuziba mianya hiyo.

Baadhi ya mianya iliyobainika katika ufuatiliaji wa usimamizi wa vyama vya msingi ni pamoja na vyama vingi kutokuwa na wataalam wa masuala ya fedha hivyo wajumbe/wanachama miongoni mwao ndio wanatumika kama wahasibu hii ni changamoto kwakuwa wengi wao hawatunzi kumbukumbu za mahesabu na kusababisha upotevu wa fedha ama ubadhirifu, pia maafisa ushirika kutotembelea mara kwa mara AMCOS zao kuona kama zinajiendesha kwa mujibu wa sheria na hivyo kupelekea bodi au uongozi wa AMCOS kuendesha ushirika kwa mazoea bila kufuata taratibu, na viongozi wengi wa AMCOS hupatikana kwa njia za Rushwa wakati wa uchaguzi. Na katika eneo la Mamlaka za barabara vijijini tulibaini Wajumbe wa kamati ya tathmini kujirudia mara kwa mara na hivyo kukosa uadilifu kwa kufanya kazi kwa mazoea. Na pia Wakandarasi kupewa kazi nyingi kwa wakati mmoja na hivyo kushindwa kutekeleza kazi kwa wakati.

**UFUATILIAJI WA MIRADI**

**Ndugu waandishi wa habari,**

Mtakumbuka kuwa ni jukumu la TAKUKURU kuhakikisha kuwa miradi ya maendeleo katika nchi yetu inakuwa na tija na kuleta matunda yaliyokusudiwa. Katika robo hii ya mwaka tumekagua jumla ya miradi ya maendeleo 11 katika sekta za elimu, ujenzi, fedha, kilimo, huduma za jamii, majengo, umeme, maji, utawala, barabara na Afya. Miradi hiyo ina thamani ya shilingi **Bilioni kumi na moja, milioni mia moja sitini na moja laki nne na elfu ishirini mia mbili ishirini na tisa na senti arobaini na tano (Shilingi 11,161,420,229.45).** Aidha katika ufuatiliaji wa miradi hiyo baadhi ya miradi ilibainika kuwa na mapungufu yaliyotokana na ukiukwaji wa taratibu za manunuzi ya umma, na baadhi ya wazabuni kulipwa malipo bila kukata kodi ya serikali (Witholding Tax) na hivyo kuikosesha mapato serikali. Wakurugenzi wa Halmashauri husika wameelekezwa kukata fedha hizo na kuahidi kuchukua hatua. Na baadhi wameshaanza kuchukua hatua.

Aidha katika Shule ya Sekondari ya ABDALAH ULEGA tulibaini kuwekwa mbao laini (softwood) katika “fremu” za madirisha kinyume na mkataba ulimtaka kutumia mbao ngumu (Hardwood). Wakati mkataba ulikuwa mbao ngumu hivyo kama angelipwa fedha ya mbao ngumu ingekuwa ni hasara. Tayari tumeshamuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri husika kuchukua hatua.

**MIKAKATI YETU KWA KIPINDI CHA JULAI MPAKA SEPTEMBA 2020**

Kama ilivyo dira ya Taifa kuelekea uchaguzi mkuu wa Rais, wabunge na madiwani mwaka huu, mikakati ya mkoa wa Pwani ni kuhakikisha uchaguzi huu unafanyika pasipokuhusisha vitendo vya Rushwa kwa kufanya yafuatayo;

- Kufikisha elimu ya madhara ya Rushwa kwa wananchi wote mpaka ngazi ya kijiji ili waone umuhimu wa kuchagua viongozi waadilifu watakaokuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi wakati wa uchaguzi.

- Kufanya uchunguzi wa tuhuma mbalimbali zinazotufikia, zikiwemo tuhuma za rushwa katika Uchaguzi kwa lengo la kupata ushahidi.

**WITO WA TAKUKURU KWA WANANCHI**

**Ndugu waandishi na wananchi,**

Naomba kutumia fursa hii kuwasihi wananchi wa mkoa wa Pwani na watanzania kwa ujumla kutumia haki yao ya kupiga kura kwa kuchagua viongozi wasiojihusisha na vitendo vya Rushwa. Aidha mwananchi unaweza kutoa taarifa za vitendo vya Rushwa TAKUKURU kupitia namba za BURE 113 AU kwa ujumbe mfupi wa simu kwa kupiga *113# kisha fuata maelekezo.

***Asanteni kwa kunisikiliza!***

***Imetolewa na***:

**Suzana Raymond-0738 150176**

**MKUU WA TAKUKURU (M)**
**PWANI**